# *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

## 1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 SEPTEMBA, 2025 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 SEPTEMBA, 2025

### 1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 01-10 SEPTEMBA, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilidumisha mwenendo wa ukandamvua kuelekea kaskazini zaidi, nje ya nchi yetu. Kwa upande mwingine Joto la bahari katika eneo la kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi (Kusini mashariki mwa Afrika) liliendelekuwa la chini ya wastani na hivyo kudumisha uwepo wa mgandamizo mkubwa wa hewa ambao ulidhohofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, upepo wenye unyevunyevu uliovuma kutoka baharini kuelekea baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani uliimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

### 1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 SEPTEMBA, 2025

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea uwepo wa vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache ya ukanda wa pwani. Maeneo mengine ya nchi yalikua makavu kwa ujumla.

## 2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 SEPTEMBA, 2025

### 2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 SEPTEMBA, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kudumisha uwepo wa ukandamvua kaskazini zaidi, nje ya nchi yetu. Kwa upande mwingine Joto la bahari katika eneo la kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi (Kusini mashariki mwa Afrika) linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani na hivyo kudumisha uwepo wa

mgandamizo mkubwa wa hewa ambao unatarajiwa kudhohofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, makutano ya upepo katika maeneo yanayozunguka Ukanda wa Ziwa Victoria, pamoja na uwepo wa upepo wenye unyevunyevu uvumao kutoka baharini kuelekea baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani vinatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

**2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 SEPTEMBA, 2025**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hasa katika kipindi cha pili cha dekad.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Hali ya ukavu inatarajiwa.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Hali ya ukavu inatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Hali ya ukavu inatarajiwa.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache hasa katika kipindi cha pili cha dekad.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Hali ya ukavu inatarajiwa.

Imetolewa na:

***MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA***

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727F – 02/2023*